**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MWENENDO WA UGONJWA UNAOSABABISHWA NA KIRUSI CHA CORONA (Novel Corona Virus 2019-nCoV) ULIOIKUMBA NCHI YA CHINA NA MATAIFA MENGINE DUNIANI.

**Ndugu Wanahabari,**

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, inaendelea kutoa tahadhari kwa umma kuhusu maendeleo ya mlipuko wa ugonjwa wa Homa kali ya Mapafu inayosababishwa na kirusi aina ya '*Corona'* ulioikumba nchi ya China na nyingine kadhaa. Ugonjwa huu umekuwa ukisambaa kwa kasi sana ambapo kumekuwa na ongezeko la wagonjwa pamoja na vifo katika kipindi kifupi kwa wastani wa zaidi ya wagonjwa 200 kwa siku.

Kwa mujibu wa taarifa rasmi kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO), tangu mlipuko wa ugonjwa huu uanze katika mji wa **Wuhan** uliopo katika jimbo la **Hubei** nchini China mwezi Disemba, 2019 hadi 28 Januari, 2020 jumla ya watu 4,593 wamethibitishwa kuugua ugonjwa huu duniani kote, ambapo kati yao wagonjwa 4,537 na vifo 106 vimetokea nchini China.

Aidha, ugonjwa huu umesambaa katika mataifa mengine 14 duniani zikiwemo Japan, Jamhuri ya Korea, Vietnam, Sangapore, Australia,

Malaysia, Cambodia, Thailand, Nepal, Sri Lanka, Marekani, Canada, Ufaransa na Ujerumani.

Vilevile kwa mujibu wa taarifa kutoka Shirika la Afya Duniani kanda ya Afrika, walioripotiwa washukiwa katika bara la Afrika wanaoendelea kufuatiliwa na kufanyiwa uchunguzi katika nchi za IvoryCost, Ethiopia, Mauritius, Kenya na Zimbabwe. Tutatolea taarifa rasmi baada ya uthibitisho kufanyika.

**Ndugu Wanahabari,**

Ugonjwa huu unasababishwa na kirusi jamii ya Corona na ni kipya **"Novel (New) Corona virus 2019"** (**2019-nCOV)** ambacho ni tofauti na virusi vingine vya jamii hiyo ambavyo viliwahi kusababisha milipuko ya ugonjwa uliojulikana kama '*SARS-CoV'* mwaka 2003 na MERS-CoV Corona Virus mwaka 2013.

Ugonjwa huu huambukizwa kwa njia ya hewa kwa kuingiwa na majimaji yenye virusi kutoka mtu mmoja kwa njia ya kukohoa au kupiga chafya au kwa kugusa majimaji au makamasi kutoka kwa mgonjwa aliyethibitishwa kuwa na dalili za ugonjwa huo na dalili huanza kuonekana kati ya siku moja hadi kumi na nne tangu kupata maambukizo.

**Ndugu Wanahabari,**

**Dalili za ugonjwa huu** ni pamoja na; **Homa, mafua, kuumwa kichwa, mwili kuchoka, kikohozi, kubanwa mbavu, maumivu ya misuli, vidonda vya koo, mapafu kuathirika, kupumua kwa shida** na hata kifo. **Ugonjwa huu hauna chanjo wala tiba ya moja kwa moja,** hivyo kama yalivyo magonjwa mengine yanayosababishwa na virusi, matibabu hufanyika kwa kuzingatia dalili zilizopo na ufuatiliaji wa karibu.

**Ndugu Wanahabari,**

**Mpaka sasa Tanzania haina Mgonjwa wala muhisiwa wa ugonjwa huu.** Hata hivyo, kutokana na mwingiliano mkubwa uliopo hasa kibiashara na kijamii kati ya Tanzania na nchi za bara la Asia ikiwemo nchi ya China nchi yetu inakuwa katika hatari pia ya ugonjwa huo.

Hivyo, Wizara inapenda kutoa tahadhari kwa wananchi wote hususani ambao wanasafiri kwenda Mataifa yaliyoathirika na mlipuko wa ugonjwa huo na wale wanaopokea wageni kutoka katika nchi hizo. **Wananchi wote wanashauriwa kuchukua hatua zifuatazo ili kujikinga na ugonjwa huu**:

1. Kuzingatia kanuni za afya na usafi ikiwa ni pamoja na kukaa mbali na mtu mwenye dalili za mafua mwenye historia ya kusafiri katika nchi zilizokumbwa na mlipuko au mwenye dalili zilizotajwa hapo juu
2. Kutokana na mwenendo na kasi ya kusambaa kwa ugonjwa huo kipindi hiki cha mlipuko, Wizara inashauri kusubiri na kuepuka safari zisizo za lazima kwenda kwenye maeneo yaliyoathirika na inapolazimu kusafiri basi wapate maelezo ya kitaalamu kabla ya kuondoka nchini
3. Kufunika mdomo na pua wakati wa kukohoa kwa kitambaa safi au nguo uliyovaa sehemu za mikono
4. Kuepuka kugusana na mgonjwa mwenye dalili za magonjwa ya njia ya hewa
5. Kuzingatia usafi binafsi ikiwemo kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni
6. Kuwahi kwenye kituo cha kutolea huduma za afya endapo utakuwa na dalili zilizoainishwa

7. Toa taarifa ya uwepo wa mtu mwenye dalili zinazohiswa kuwa za ugonjwa huu kwenye kituo cha huduma za afya kilicho karibu nawe au piga simu namba 0800110124 au 0800110125 bila malipo.

**Ndugu Wanahabari,**

**Serikali kupitia Wizara ya Afya imechukua hatua zifuatazo** katika kukabiliana na tishio la ugonjwa huu:

1. Kuendelea kuimarisha ufuatiliaji wa ugonjwa huu kwenye mipaka yetu na vituo vyote vya huduma ambapo watoa huduma wanazingatia na kuwa makini zaidi kwenye uchunguzi hasa kwa watu wanaotoka nje ya nchi
2. Kufanya uchunguzi wa wasafiri wote kutoka bara la Asia kwenye mipaka yetu ikiwemo viwanja vya ndege vya Mwalimu Julius Nyerere, Kilimanjaro na Mwanza; na bandari ya Dar es Salaam, mfano kwa kipindi cha wiki mbili zilizopita, tumefanya uchunguzi wa raia **1520** waioingia nchini kutokea China na Asia kupitia mipakani na viwanja vya ndege. Aidha, tumeanza kufanya uchunguzi wa abiria kwa ndege zote zinazoingia nchini
3. Wizara inavyo vipima joto 140 (vya mkono 125 na vya kupima watu wengi kwa mpigo 15) ambavyo vimefungwa na vinatumika katika maeneo yetu ya mipakani ikiwemo viwanja vya ndege na bandari

4. Katika ufuatiliaji wa ugonjwa huu na magonjwa mengine ya aina hiyo Wizara inaendelea kuchukua na kupima sampuli kutoka maeneo ya ufuatiliaji na yeyote atakayehisiwa kuwa na dalili za ugonjwa huu sampuli zitafikishwa kwenye maabara ya Taifa kupimwa

5. Kutoa taarifa ya tahadhari ya ugonjwa huu kwenye Mikoa na Halmashauri zote nchini na kuwataka Waganga Wakuu wote wa Mikoa na Halmashauri kuchukua tahadhari na kuimarisha ufuatiliaji na mbinu ya kukinga maambukizi katika maeneo yao ikiwemo mipakani kwa kuzingatia miongozo iliyopo.
6. Kuandaa maeneo maalumu ya matibabu kwa wagonjwa endapo watajitokeza. Maeneo yaliyoainishwa ni Mawenzi (Kilimanjaro), Buswelu (Mwanza) na Kigamboni (Dar es Salaam).
7. Wizara inaendelea kujiandaa kukabiliana na tishio la Ugonjwa huu kwa kuhakikisha tunapata vifaakinga, dawa na vifaa tiba vya kutosha kukabiliana na ugonjwa huu endapo utaingia nchini

8. Kuendelea kutoa elimu kwa njia mbalimbali ili wananchi na watoa huduma kuchukua tahadhari

9. Pia tumetoa mafunzo kwa watumishi wa sekta ya afya katika kukabiliana na magonjwa ya milipuko na majanga ikiwemo jinsi ya kutoa matibabu ya magonjwa ya milipuko, kuchukua sampuli, uelimishaji na kufuata kanuni za afya. Mpaka sasa watumishi 2,297 wamekwishapatiwa mafunzo.

**Ndugu Wanahabari,**

Nimalizie kwa kusema kuwa hapa nchini hadi sasa hakuna mgonjwa wala mtu yeyote anayehisiwa kuwa na ugonjwa unaosababishwa na Virusi vya *novel Corona*. Hivyo Wananchi wanashauriwa kutokuwa na hofu, waendelee kuchukua hatua za tahadhari katika kujikinga na ugonjwa huu na kutosambaza taarifa zisizothibitishwa na Wizara. Aidha, ninaviomba vyombo vya habari kuhakikisha mnawafikishia wananchi wa Tanzania taarifa sahihi na elimu juu ya ugonjwa huu.

Katika kuhakikisha afya ya Watanzania inalindwa na kudumishwa, Serikali itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa sekta ya afya, likiwemo Shirika la Afya Duniani (WHO).

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**

**IMETOLEWA NA:**

**UMMY MWALIMU (MB)**
**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO.**
**29 JANUARI, 2020**